TANGAZO LA SERIKALI NA. 778 la tarehe 3/11/2023

# SHERIA YA USIMAMIZ NA TOZO YA USHURU

(SURA YA 147)

# AMRI

(*Imetolewa chini ya kifungu cha 128*)

## AMRI YA MSAMAHA WA USHURU WA BIDHAA KWA MAGARI MATATU YA MRADI WA KUDHIBITI SUMUKUVU NCHINI WA WIZARA YA KILIMO YA MWAKA 2023

Jina na kuanza kutumika

1. Amri hii itajulikana kama Amri ya Msamaha wa Ushuru wa Bidhaa kwa Magari Matatu ya Mradi wa Kudhibiti Sumukuvu Nchini wa Wizara ya Kilimo ya mwaka 2023 na itaanza kutumika kuanzia tarehe 23 Agosti, 2023.

Msamaha

2. Kwa kuzingatia masharti yaliyoainishwa katika aya ya 3, na masharti mengine yoyote yanayoweza kuimarishwa na Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato Tanzania, kiasi chote cha ushuru wa bidhaa kinachotakiwa kulipwa kuhusiana na magari matatu yaliyoanishwa kwenye Jedwali, yanayoingizwa au kununuliwa ndani ya nchi, kabla ya kibali cha forodha na kwa niaba ya Wizara ya Kilimo, kwa ajili ya kutumiwa mahususi katika utekelezaji wa Mradi wa Kudhibiti Sumukuvu, kimesamehewa.

Masharti

3. Msamaha wa kodi unaotolewa chini ya Amri hii utafikia ukomo na ushuru utadaiwa na utatakiwa kulipwa kana kwamba msamaha chini ya Amri hii haukutolewa, iwapo magari husika yatatumika kwa matumizi tofauti au yatahamishwa, kuuzwa au kwa

namna yoyote atapewa mtu mwingine asiyestahili kufaidika na faida zinazotolewa chini ya Amri hii.

Kuisha kwa muda

4. Msamaha uliotolewa chini ya Amri hii utafika ukomo tarehe 27 Disemba, 2023.

JEDWALI

*(Limetengenezwa chini ya aya ya* 2)

| Na. | Maelezo | Chasis Na. | Idadi |
|---|---|---|---|
| 1. | Toyota Hilux D/Cabin1GD 2.8L 4WD | AHTKA3CD30-5312910 | 1 |
| 2. | Toyota Hilux D/Cabin1GD 2.8L 4WD | AHTKA3CD70-5312909 | 1 |
| 3. | Toyota Land Cruiser Prado TXL Manual | JTEBR3FJ90-K292411 | 1 |

Dodoma,
19 Octoba, 2023

MWIGULU LAMECK NCHEMBA MADELU
*Waziri wa Fedha*